

Hojaji ya Kukusanya Taarifa za Makazi ya



MADHUMUNI YA HATI HII:

Hojaji hii inakusudiwa kushughulikia Sheria ya Utoaji Msaada wa Elimu ya McKinney-Vento 42 U.S.C. 11431. Majibu ya hojaji hii yanasaidia kubainisha ikiwa mwanafunzi wako anastahiki huduma na/au nyenzo za ziada.

MAELEKEZO

Tafadhali jaza fomu hii kikamilifu na kwa usahihi, irejeshe kwa shule ambayo ungependa kujiandikisha au itume kwa Mwasiliani wa Elimu, mike.harman@slcschools.org; Salt Lake City School District, 440 East 100 South, 84111, au itume kwa faksi kwa 801-578-8583.

MAELEZO YA MWANAFUNZI

Jina la Mwanafunzi

Nambari ya Mwanafunzi

Jinsia

Mwanaume Mwanamke

Shule

Darasa

HOJAJI

1. Tafadhali onyesha ni gani, ikiwa yoyote ipo, kati ya hali zifuatazo za muda zinazomhusu mwanafunzi wako:

- 1401 Mwanafunzi anaishi **kwa muda** pamoja na familia moja au zaidi kwa sababu ya kupoteza makazi, ugumu wa kiuchumi au sababu kama hiyo.
- 1402 Mwanafunzi anaishi katika moteli au hoteli.
- 1403 Mwanafunzi anaishi katika makazi yanayowapa watu hifadhi ya muda (kitengo cha makazi ya watu wanaopitia unyanyasaji nyumbani, waliokumbwa na hali za dharura au makazi ya kipindi cha mpito).
- 1404 Mwanafunzi anaishi katika gari, bustani, uwanja wa kambi au mahali pa umma.
- 1405 Mwanafunzi anaishi mahali **ambapo hapana** vifaa vya kutosha kwa ajili ya kutoa huduma za kimsingi (hakuna huduma za maji ya bomba, mifumo ya kupasha joto kwenye nyumba, na/au umeme).
- Hakuna zinazomhusu kati ya hizi. (Huhitaji kujibu maswali ya 2-3 lakini tafadhali tia sahihi ya uthibitisho hapa chini)

2. Tafadhali eleza kwa ufupi hali ya mazingira ya sasa unamoishi: _____

3. Je, huyo mwanafunzi anaishi na mzazi au mlezi wake wa kisheria? (bila kujumuisha mipango ya utunzaji wa watoto iliyoidhinishwa na serikali na uangalizi wa watoto na serikali ya jimbo)

Ndiyo Hapana, ikiwa ni hapana, tafadhali eleza: _____

Tafadhali kumbuka:

- Ikiwa dai la uwongo litatolewa kuhusu hali ya mazingira unamoishi, mchakato wa uandikishaji unaweza kuathiriwa.
- Tafadhali ijulishe shule ikiwa hali ya mazingira unamoishi itabadilika.

SHUKURANI

Sahihi ya Mzazi/Mlezi (Kijana Asiye na Mlezi).

Tarehe

Hakuna mwajiriwa au mwanafunzi wa wilaya atakayebaguliwa katika ajira au mpango au shughuli yoyote ya wilaya kwa misingi ya umri, rangi, ulemavu, jinsia, utambulisho wa kijinsia, taarifa za vinasaba, uraia, ujauzito, mbari, dini, mwelekeo wa kijinsia, au hali ya mstaafu. Wilaya imedhamiria kutoa ufikiaji sawa na fursa sawa katika mipango yake, huduma na ajira ikiwemo sera zake, michakato ya malalamiko, ufikiaji wa mipango, matumizi ya huduma za wilaya, malazi na masuala mengine ya Nafasi Sawa za Ajira. Wilaya pia inatoa ufikiaji sawa kwa huduma za wilaya kwa makundi yote ya vijana yaliyoorodheshwa katika Title 36 ya Sheria ya Marekani, ikiwemo makundi ya skauti. Mtu huyu amechaguliwa kushughulikia maswali na malalamiko kuhusu ubaguzi, unyanyasaji, na ulipizaji kisasi ulio kinyume cha sheria: Tina Hatch, Uzingatiaji na Uchunguzi, 440 East 100 South, Salt Lake City, Utah 84111, (801) 578-8388. Unaweza pia kuwasiliana na Ofisi ya Haki za Kirai, Denver, CO, (303) 844-5695.